**DONDOO ZA MWENYEKITI WA TUME YA RAIS YA KUCHUNGUZA MATUKIO YA GHASIA NA UVUNJIFU WA AMANI YALIYOTOKEA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU WA OKTOBA 2025 WAKATI AKIONGEA NA WANAHABARI WA VYOMBO VYA HABARI TAREHE 01 DESEMBA 2025**

---

**Wahe. Wajumbe wa Tume,**

**Ndugu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali,**

**Ndugu Wanahabari,**

## UTANGULIZI

**Ndugu Wanahabari,**

1. Itakumbukwa kuwa, tarehe 29 Oktoba 2025 ulifanyika Uchaguzi Mkuu nchini uliohusisha uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na madiwani wa Tanzania Bara. Uchaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayoelekeza kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu kila baada ya kipindi ya miaka mitano (5).

**CHIMBUKO LA KUUNDWA KWA TUME**

**Ndugu Wanahabari,**

2. Kama mnavyofahamu, katika siku ya uchaguzi na takriban siku tatu zilizofuatia zilitokea ghasia zilizoambatana na vitendo vya uvunjifu wa amani katika baadhi ya maeneo ya miji nchini ikiwemo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Songwe, Mara na Geita. Vitendo hivyo vilisababisha vifo; majeruhi; uporaji; uharibifu wa miundombinu na mali za umma pamoja na mali za watu binafsi.

3. Kufuatia hali hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 20 Novemba, 2025 aliunda na kuzindua Tume Huru ya kuchunguza matukio ya ghasia na uvunjifu wa amani yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi. Tume hii imeundwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume za Uchunguzi Sura ya 32, Toleo la mwaka 2023.

**WAJUMBE WA TUME**

**Ndugu Wanahabari,**

4. Tume iliyoundwa ina Wajumbe 9 ikiongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania, Mohamed Othman Chande. Wajumbe wa Tume ni Profesa Ibrahim Juma, Jaji Mkuu Mstaafu wa Mahakama ya Tanzania; Balozi Ombeni Sefue, Mwanadiplomasia na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu; Balozi Radhia Msuya, Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu; Balozi Luteni Jenerali Paul Meela, Balozi Mstaafu George Madafa; Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu; Said Mwema, Mkuu wa Jeshi la Polisi Mstaafu; Balozi David Kapya, Mwanadiplomasia na Balozi Mstaafu; Dkt.

Stergomena Tax, Waziri Mstaafu na aliyewahi kuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Aidha, uteuzi wa wajumbe hawa umezingatia masharti ya Sheria ya Uchunguzi, Sura ya 32 yanayompa Rais mamlaka ya kuagiza uchunguzi katika jambo lolote ambalo anaona lina manufaa kwa umma.

**MADHUMUNI YA TUME**

**Ndugu Wanahabari,**

5. Lengo kuu la kuundwa kwa Tume ni kuchunguza kwa kina kiini cha ghasia zilizojitokeza wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu. Lengo hilo linaakisi Hadidu za Rejea zilizotolewa kwa Tume ambazo zinajikita katika nguzo tano za kiuchunguzi ambazo ni: chanzo cha ghasia, wahusika, madhara, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuzuia na kudhibiti matukio ya uvunjifu wa amani. Aidha, pamoja na mambo mengine, Tume itapendekeza maeneo yanayohitaji kuimarishwa zaidi ili kuongeza uwajibikaji wa viongozi na raia kwenye kulinda amani, utawala wa sheria, haki za binadamu, utawala bora na mfumo madhubuti wa majadiliano ya kisiasa, kijamii na kiuchumi hadi kufikia maridhiano ya kitaifa na kuhakikisha vurugu kama hizi hazitokei tena.

**HADIDU ZA REJEA**

**Ndugu Wanahabari**

6. Katika kutekeleza majukumu yake Tume itaongozwa na Hadidu za Rejea zifuatazo:

6.1. Kuchunguza na kubainisha chanzo halisi cha ghasia zilizotokea wakati wa Uchuguzi Mkuu nchini uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 na siku chache zilizofuata;

6.2. Kuchunguza lengo kuu lililokusudiwa na waliohusika katika kupanga na kutekeleza vitendo hivyo vya ghasia na uvunjifu wa amani;

6.3. Kuchunguza na kubainisha madhara yaliyojitokeza kutokana na ghasia hizo ikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu na madhara ya kiuchumi na kijamii;

6.4. Kuchunguza mazingira na hatua zilizochukuliwa katika kubaini na kukabiliana na ghasia zilizojitokeza;

6.5. Kupendekeza maeneo yanayohitaji kuimarishwa zaidi ili kuongeza uwajibikaji wa viongozi na raia kwenye kulinda amani, utawala wa sheria, haki za binadamu, utawala bora na mfumo madhubuti wa majadiliano ya kisiasa, kijamii na kiuchumi hadi kufikia maridhiano ya kitaifa na kuhakikisha vurugu kama hizi hazitokei tena; na

6.6. Kuchunguza jambo lolote ambalo Tume itaona kuwa ni muhimu na linaendana na majukumu ya Tume.

**MAWANDA YA KAZI**

**Ndugu Wanahabari,**

7. Katika kutekeleza majukumu yake, Tume itazingatia masharti ya Sheria ya Tume za Uchunguzi na utaratibu itakaojiwekea kwa

mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Tume za Uchunguzi. Uchunguzi wa Tume utahusisha maeneo yaliyoathirika zaidi na ghasia kwa upande wa Tanzania Bara ili kubaini aina ya matukio, chanzo, athari na hatua zilizochukuliwa katika kuzuia na kudhibiti hali hiyo. Vilevile, itatembelea baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa na ghasia ili kujifunza mazingira yaliyochangia hali hiyo.

8. Sheria ya Tume ya Uchunguzi inaipa mamlaka Tume ya kumwita au kumwalika mtu yeyote kwa ajili ya mahojiano kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia katika uchunguzi. Hivyo, tunatoa wito kwa watanzania wote kutoa ushirikiano ili Tume iweze kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

9. Sheria ya Tume ya Uchunguzi pia inaipa mamlaka Tume kuamua juu ya taratibu (rules of procedure) zitakazotumika. Tume pia imepanga kufanya baadhi ya mahojino yake na wadau mbalimbali na Wataalamu kwa njia ya wazi (*public hearings*).

**METHODOLOJIA**

**Ndugu Wanahabari,**

10. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mawanda mapana, Tume itatumia njia mbalimbali zitakazowezesha kupata taarifa sahihi na za kina. Njia hizo zitajumuisha mapitio na uchambuzi wa nyaraka mbalimbali, mahojiano ya ana kwa ana na kwa njia ya mitandao, dodoso la mtandaoni, barua pepe, barua za kawaida, ujumbe mfupi wa simu, kutembelea uwandani, mijadala ya makundi mbalimbali na ushauri wa kitaalam. Ni imani yetu

kuwa, kwa kutumia njia zote hizi tutaweza kupata taarifa zote muhimu na tutawafikia wadau walio wengi.

**WADAU WATAKAOSHIRIKISHWA**

**Ndugu Wanahabari,**

11. Wadau watakaoshirikishwa watatoka katika makundi mbalimbali ya jamii. Baadhi ya wadau hao ni; waathirika; watuhumiwa; vyama vya siasa; asasi za kiraia; wasimamizi wa uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi; viongozi wa dini; viongozi wa bodaboda; viongozi wa machinga, wafanyabiashara na wajasiriamali, washirika wa maendeleo; watu mashuhuri; mamlaka za serikali za mitaa hasa kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi Wakuu wa Taasisi za Serikali; Vyombo vya ulinzi na usalama na sekta binafsi za ulinzi; waandishi wa Habari, watafiti na wataalamu wa sekta na fani mbalimbali.

**MUDA WA KAZI**

**Ndugu Wanahabari,**

12. Kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais, Tume inatarajia kukamilisha kazi yake ndani ya muda wa siku 90 tangu ilipozinduliwa ili kukamilisha kazi na kuwasilisha taarifa kwa Mhe. Rais. Hivyo, kuanzia sasa Tume ipo tayari kupokea taarifa na maoni kupitia Tovuti ya Tume kwa anuani ya ***https://www.tume.uchunguzi.go.tz*** barua pepe, ***maoni@tume.uchunguzi.go.tz,*** Simu na ujumbe mfupi kupitia namba Vodacom: 0743 040 890 au TTCL: 0737 305 449

**HITIMISHO**

**Ndugu Wanahabari,**

13. Napenda kuwahakikishia kuwa, Tume ni hii ni huru kabisa kwa mujibu wa sheria, na imeelewa vyema majukumu yake na inatambua uzito wake. Hivyo, ahadi yetu ni kutekeleza majukumu hayo kwa weledi, uadilifu na uwazi ili kuleta majibu sahihi. Ninatoa rai kwa vyombo vya habari na wananchi wote kutoa ushirikiano kwa Tume kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza

***************************